

Mapishi ya wali kuku wa Kisomali

By SW - Melkisedeck Shine · September 26, 2022

Dondoo za Mapishi na Lishe · Upishi na Maandalizi ya Milo yenye Afya · #Karibu AckySHINE

Mahitaji ya wali

Mchele - 3 vikombe

Vitunguu (viliokatwa vidogo vidogo) - 2

Mafuta - 3 vijiko vya supu

Kitunguu saumu(thomu/galic) na tangawizi iliyosagwa - 1 kijiko cha chai

Bizari ya pilau - 1 kijiko cha supu

Mdalasini - 1 kijiti

Hiliki - 3 chembe

Pilipili manga nzima - chembe chache

Siagi - Vijiko 2 vya supu

Chumvi - kiasi

Mahitaji kwa kuku

Kuku kidari (Breast) kata vipande vipande - 2 LB

Mafuta - 3 vijiko vya supu

Kitunguu saumu(thomu/galic) na tangawizi iliyosagwa - 1 kijiko cha supu

Pilipili mbichi iliyosagwa - 1 kijiko cha supu

Kotmiri iliyokatwa ndogo ndogo - kiasi

Bizari ya pilau (cummin au jiyrah) - 1 kijiko cha chai

Pilipili kubwa tamu la kijani - 1

Pilipili kubwa tamu nyekundu - 1

(zikate vipande vipande)

Chumvi - Kiasi

Mapishi ya Wali:

Roweka mchele kwa muda fulani kutegemea mchele Katika sufuria tia mafuta na kaanga vitunguu hadi vibadilike rangi kidogo. Tia thomu iliyosagwa, mdalasini, bizari ya pilau, hiliki, pilipili manga na chumvi, kaanga kidogo. Tia mchele kaanga kidogo, kisha tia maji ya moto kiasi kutegemea na aina ya mchele kama kawaida ya kupika wali kama pilau. Tia sigai, funika upikike wali hadi uwive.

Mapishi ya Kuku:

Mchanganye kuku pamoja na thomu/tangawizi iliyosagwa, chumvi, pilipili mbichi. Katika karai tia mafuta yapate moto vizuri. Mtie kuku, bizari ya pilau (jiyrah) na ukaange, karibu na kuiva tia vitunguu. Tia mapilipili makubwa, kotmiri, na kaanga kwa dakika moja tu uzime moto na epua weka kando.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=24306>